

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**



**MKUTANO WA SITA**

**KIKAO CHA SITA**

**08 FEBRUARI, 2022**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA SITA

**KIKAO CHA SITA – TAREHE 08 FEBRUARI, 2022**

#### **I. DUA:**

#### **II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

##### **WAZIRI MKUU:**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na.45 la tarehe 05 Novemba, 2021;
2. Toleo Na.46 la tarehe 12 Novemba, 2021;
3. Toleo Na.47 la tarehe 19 Novemba, 2021;
4. Toleo Na.48 la tarehe 26 Novemba, 2021;
5. Toleo Na.49 la tarehe 03 Desemba, 2021;
6. Toleo Na.50 la tarehe 10 Desemba, 2021;
7. Toleo Na.51 la tarehe 17 Desemba, 2021;
8. Toleo Na.52 la tarehe 24 Desemba, 2021;
9. Toleo Na.53 la tarehe 31 Desemba, 2021;
10. Toleo Na.01 la tarehe 07 Januari, 2022;
11. Toleo Na.02 la tarehe 14 Januari, 2022;

12. Toleo Na.03 la tarehe 21 Januari, 2022; na
13. Toleo Na.04 la tarehe 28 Januari, 2022.

### **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu wa Mwaka 2022 (*The Anti - Money Laundering (Amendment) Bill, 2022*)

### **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu wa Mwaka 2022, (*The Anti - Money Laundering (Amendment) Bill, 2022*).

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA WAZIRI MKUU:**

#### **54. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali inachukua hatua gani ya kuwawezesha Wahitimu wa Vyuo Vikuu ambao hawana ajira kulipa mikopo yao.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**55. MHESHIMIWA SHABANI OMARI SHEKILINDI (LUSHOTO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka Watumishi wa kada ya Ualimu na Afya katika Wilaya ya Lushoto.

**56. MHESHIMIWA KASSIM IDDI IDDI (MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatoa Vifaa Tiba na Dawa za kutosha kwenye Vituo vya Afya na Zahanati zote katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala.



**57. MHESHIMIWA CONCHESTA LEONCE  
RWAMLAZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni kuwa kuajiri walimu bila kujali muda wa kuhitimu, baadaye baadhi yao wataashindwa kuajiriwa kutokana na umri wao kuwa mkubwa.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA  
MAZINGIRA):**



**58. MHESHIMIWA RASHID ABDALLA RASHID  
(KIWANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, ni lini Serikali itajenga tuta la kuzuia maji ya Bahari yanayoharibu mashamba ya Wananchi wa Vijiji vya Nanguli, Jundamiti, Mwambe na Kiwani katika Jimbo la Kiwani.

**WIZARA YA NISHATI:**

**59. MHESHIMIWA FRANCIS LEONARD MTEGA  
(MBARALI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha kuvipatia umeme wa REA Vitongoji na Vijiji vilivyobaki katika Jimbo la Mbarali.

**60. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Umeme wa REA kama ilivyoahidi katika Vijiji vya Kitayawa, Kipera, Lupalama, Itagutwa, Ikungwe na Lyamgungwe.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**61. MHESHIMIWA DANIEL BARAN SILLO  
(BABATI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-


Je, ni lini Serikali itasaidia ujenzi wa Kituo cha Polisi Galapo Tarafa ya Babati ambacho kinajengwa kwa nguvu za Wananchi.

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:**

**62. MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Viwanda vya kusindika Maziwa katika Mkoa wa Arusha.



**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**63. MHESHIMIWA BERNADETA KASABAGO MUSHASHU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni lini Wananchi waliokuwa wameweka Fedha zao katika Benki ya Wakulima wa Kagera ya

KFCB iliyofungwa na Benki Kuu Mwaka 2018 watarejeshewa Fedha zao.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**64. MHESHIMIWA ATHUMAN ALMAS MAIGE  
(TABORA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya  
● Tabora – Mambali – Ishihimulwa – Shitage – Mhulidede kwa kiwango cha lami.

**65. MHESHIMIWA SALIM MUSSA OMAR  
(GANDO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, nini kinasababisha mabadiliko makubwa ya bei za tiketi za Ndege za Air Tanzania kwa safari za Dar es Salaam na Dodoma ambapo mara nyingi hufika hadi Shilingi laki sita.



## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**66. MHESHIMIWA NEEMA GERALD  
MWANDABILA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,  
Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itajenga Vyuho Vikuu katika  
Mkoa wa Songwe.

### IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***[Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge  
Zima na Kusomwa Mara ya Tatu]***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya  
Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu wa Mwaka  
2022 (*The Anti – Money Laundering (Amendment)  
Bill, 2022*).

**DODOMA  
08 FEBRUARI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**